BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 01 Juni, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu kwa mwaka 2026/2027.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Ardhi na Tehama:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Miundombinu, Ardhi na Tehama kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu kwa mwaka 2026/2027.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

79. MHESHIMIWA MAHFOUDH ABDALLA MOHAMMED (Jimbo Magomeni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

    Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2024, asilimia 77 (77%) ya Watanzania wamezaliwa baada ya Muungano, hivyo uelewa wao wa sababu, umuhimu na fursa za Muungano wetu huu ni mdogo.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutoa elimu kwa umma katika makundi mbalimbali katika jamii, ili kukuza uelewa wa Muungano wetu na kuondoa upotoshaji wa makusudi wa usahihi na nia thabiti ya waasisi wa Muungano huu.

(b) Je, Serikali imechukuwa somo gani kutokana na kuvunjika kwa baadhi ya miungano duniani kama vile Somali Republic, Senegambia na mengineyo, ili kutunza tunu hii adhimu ya taifa na kuirithisha kwa vizazi vijavyo.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

426. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa kuwa mashekhe wetu wa Unguja na Pemba wametoa mchango mkubwa katika kuendeleza elimu na maadili mema katika jamii zetu, hali ambayo imeongeza maisha ya upendo, huruma, amani na utulivu nchini.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka makumbusho ya mashekhe wetu hapa Zanzibar, ili kutunza tareikh zao na kazi zao nzuri walizofanya katika nyakati zao.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

236. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Jumbi ni miongoni mwa shehia inayokuwa kwa kasi kimakaazi ukilinganisha na miaka mingi ya nyuma, ila kuna changamoto ya wakaazi wa shehia hiyo kutojua wapi wakatupe taka zao, maana hata kuchimba shimo mbele ya nyumba pia haileti picha nzuri, kutokana na uhalisia wa mji huo pamoja na mazingira yake.

Je, Baraza la Mji la Wilaya ya Kati lina mkakati gani wa kuitatua changamoto hii na kuwaelekeza wananchi wa shehia hiyo wapi waweke taka zao.

272. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na malalamiko ya wananchi wengi wa Zanzibar juu ya utozwaji wa adhabu za papo kwa papo, pale mwananchi anapothibitika kufanya kosa linalosimamiwa na Serikali za Mitaa, hasa ukizingatia kuwa adhabu hizo zinawagusa moja kwa moja wananchi wa kipato cha chini.

Je, ni lini Serikali itafikiria kuondoa adhabu hiyo na kubuni njia mbadala ambayo itampa unafuu mwananchi wa Zanzibar.

**Wizara ya Kazi na Uwekezaji:**

348. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Taasisi binafsi ni moja ya miongoni mwa taasisi muhimu ambazo huongeza uzalishaji wa ajira kwa vijana wetu. Hata hivyo, kumekuwa na tabia ya wananchi kutopewa mikataba, kudhalilishwa na kufukuzwa kazi bila ya kufuata taratibu za uachishwaji wa kazi, hasa kampuni za ujenzi na kampuni zilizopewa dhamana ya kuendesha hospitali, huku wananchi walio wengi wakiwa na uelewa hafifu wa kutojua wapi pakukimbilia na hatua gani za kuchukua.

(a) Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuhakikisha inapunguza tatizo hili.

(b) Je, ni taasisi ngapi zimechukuliwa hatua za kinidhamu juu ya tabia hii.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

217. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Tunaipongeza Serikali yetu kwa kuleta mabasi ya umeme ambayo yatakuwa ni kivutio kizuri kwa nchi yetu.

(a) Je, ni ipi nafasi ya dala dala zetu za sasa, baada ya mabasi hayo kuanza kutumika nchini.

(b) Je, kwa kiwango gani madereva na makondakta wa dala dala zetu za sasa watazingatiwa katika ajira mpya za mabasi ya umeme.

(c) Kwa nini Serikali haikujenga njia maalumu za mabasi hayo, kama ilivyo mabasi ya mwendo kasi ya Dar es Salaam, yalivyojengewa njia maalumu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

128. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na na Mafunzo ya Amali:

Hivi karibuni kumetolewa taarifa ya Mtaala Mpya wa Elimu unaotegemewa kutumika kuanzia mwaka 2027 kwa Tanzania nzima. Hata hivyo, vipengele kadhaa katika Mtaala huo hasa kwenye masomo ya dini yanaonekana hayaendani na mahitaji ya kielimu kwa upande wa Zanzibar, ambako masomo ya dini ni muhimu kwa ajili ya kuviendeleza vyombo vya kiutumishi ndani ya Serikali kama vile Mahakama ya Kadhi, Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana na Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar. Sambamba na hilo, masomo ya dini kwa upande wa Zanzibar ni lazima, ili kuandaa wataalamu katika huduma za kifedha, kiuchumi na biashara zinazofuata misingi ya Shariah.

(a) Je, kwa namna Mtaala huo ulivyoyaweka masomo ya dini, kwa kiwango gani yanaendana na maslahi ya Zanzibar katika maeneo niliyoyataja.

(b) Je, ni ipi kauli ya Serikali katika kukubaliana na mitaala hiyo kwa upande wa Zanzibar.

(c) Je, ni upi mustakbali wa vyombo vyetu vya Kidini na miamala ya kidini endapo masomo ya dini yatawekwa kando, katika muktadha wa kuandaa wataalamu tokea ngazi za chini.

382. MHESHIMIWA DKT. MAHMOUD OMAR HAMAD (Jimbo la Tumbatu) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza walimu kwenye maeneo yenye upungufu hususani katika visiwa na mashamba.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

485. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali imejitahidi kujenga majengo ya hospitali, jambo ambalo sio baya ila huduma bado haziridhishi. Kwa mfano, unaweza ukaenda na mgonjwa ila mtu wa mapokezi akawa hayupo ama yupo msalani au anaswali huku mgonjwa hapewi huduma kwa wakati, jambo

ambalo limekuwa ni mwiba na mateso kwa wananchi.

Wananchi wanataka kujuwa, lipi la muhimu kati ya usajili wa mgonjwa na kupatiwa matibabu mgonjwa.

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

168. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI Ali (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Ukarabati wa viwanja vya michezo, Gombani kisiwani Pemba na Amani Complex Stadium kwa Unguja, ni miradi iliyochukua muda mrefu kukamilika kwake pamoja na usiri mkubwa wa matumizi ya fedha za umma zilizotumiwa katika ukarabati huo. Aidha, hadi sasa Serikali haijaweka wazi gharama halisi zilizotumika katika miradi hiyo, huku bado kukiwa na ukarabati wa mwendo wa kusuasua unaoendelea katika viwanja hivyo.

(a) Je, Serikali imetumia gharama za kiasi gani kufanya ukarabati wa uwanja wa Amani pamoja na Gombani hadi sasa.

(b) Je, Serikali iliipatia kampuni gani zabuni ya ujenzi ama ukarabati wa viwanja hivyo na kwa utaratibu upi uliotumika.

(c) Je, Serikali itatumia gharama za kiasi katika ujenzi wa kiwanja cha AFCON Fumba.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

324. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Miongoni mwa majukumu ya usambazaji wa maji ni kuhakikisha usalama na ubora wa maji yanayotolewa kwa wananchi. Katika kutekelezwa hilo hakuna budi visima vya maji vikapimwa mara kwa mara.

Je, Serikali inafanya uchunguzi wa kitaalamu wa usalama na ubora wa maji katika visima vyake.

## Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

195. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Uendelezaji wa miji ya kisasa unahitaji mipango bora ya makaazi katika nchi yetu, kitu ambacho hakijafikia malengo mahasusi kutokana na baadhi ya wasimamizi wa chini katika shehia zote za Zanzibar, kutokutoa mashirikiano kamilifu katika kufikia dhamira ya malengo hayo, kwa kuruhusu ujenzi holela na kushiriki katika uuzwaji wa baadhi ya viwanja usiozingatia utaratibu.

(a) Je, ni upi mpango mkakati wa Serikali wa kulitatua tatizo hili kwa kuweka Msimamizi wa Mipango Miji kuanzia kwenye ngazi za shehia.

(b) Kwa nini Serikali inawatambua masheha kama Mawakala wa Mauziano katika uuzwaji na ununuzi wa viwanja.

(c) Je, ni utaratibu gani unaotumiwa na Kamisheni ya Ardhi ili kuweza kutoa Hati za Matumizi ya Ardhi.

## Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:

6. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Tunaipongeza Serikali ya Awamu ya Nane kwa kasi kubwa na fanisi ya kujenga barabara mbalimbali za Unguja na Pemba, ikiwa ni pamoja na barabara za ndani. Hata hivyo, barabara ya ndani kutoka Bule kuelekea Jichwa katika jimbo la Tumbe ni mbovu kwa muda mrefu na haipitiki katika kipindi cha mvua, huku wananchi wanaoishi katika maeneo hayo wanaendelea kupata usumbufu mkubwa na kukosa raha ya maisha yao.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami au angalau kwa kiwango cha zege.

(b) Ujenzi huo utaanza na unatarajiwa kumalizika lini ili wananchi wa maeneo hayo waondokewe na usumbufu unaowakabili.

437. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Je, Serikali inafanya uchunguzi wa kuangalia ‘life jacket’ wakati wa kusafirisha abiria kwa vyombo vya baharini.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

495. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Katika jitihada za kuongeza idadi ya watalii nchini, Serikali inalazimika kuendelea kutafuta njia mbadala za kuimarisha sekta ya utalii katika visiwa vyetu ikiwemo utalii wa mikutano.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuhakikisha kisiwa cha Pemba kinakuwa kivutio cha utalii wa mikutano ili kuongeza wageni mapato na fursa za ajira kwa wananchi.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu kwa mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**01 Juni, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**WAWAKILISHI, ZANZIBAR**